CultureTalk Tanzania Video Transcripts: http://langmedia.fivecolleges.edu

Swahili as the National Language

Swahili transcript:

Kwanza kabisa napenda niwakaribishe Tanzania,Tanzania ni nchi ya amani,ni nchi ambayo iko katika Afrika ya Mashariki,na watanzania,lugha yetu ya Taifa,ambayo ni lugha ambayo inatuunganisha watanzania ni lugha ya Kiswahili.Kwa hiyo tunatumia lugha ya Kiswahili katika mawasiliano,katika mazungumzo ya kila siku,katika sehemu za kazi na hata mashuleni,majumbani na sehemu mbalimbali kama kwenye sherehe na sehemu mbalimbali ambazo jamii inakusanyika.Tunafurahi kwamba Tanzania ni nchi ya amani na ni nchi ya upendo kwa sababu watanzania wote tumeunganishwa kwa lugha hii moja,lugha ya Kiswahili.Tanzania tuna makabila yasiyopungua mia moja na ishirini ambayo yanafanya kuwa na lugha za kikabila zisizopungua mia moja na ishirini.Mbali kuwa na lugha hizo mia moja na ishirini,lugha za kikabila,lakini jamii nzima ya kitanzania tunaunganishwa na lugha moja, ya Kiswahili.Aaah!hapo ninamaanisha kwamba kwa mfano kuna lugha kama kuna makabila mengi kwa mfano kabila la wamasai,kabila la wachaga,kabila la wangoni,kabila la wajita,wasukuma na wengineo,na katika kila kabila kuna lugha ya kikabila,kwa mfano mmh!kabila la wamasai wana lugha yao ya kimasai,kabila la wachaga wana lugha yao ya kichaga,kabila la wangoni wana lugha yao ya kingoni,kabila la wasukuma wana lugha yao ya kisukuma,lakini watu hawa wote katika makabila yao na katika lugha zao wanatumia lugha ya Kiswahili pale wanapokutana pamoja.Kwa mfano aah! mchaga amekutana na msukuma,kwa vile lugha zao ni tofauti(wana)wataongea lugha ya Kiswahili ili waweze kuwasiliana,kwa sababu mmasai au mchaga akiongea kichaga,na anyeongea nae sio mchaga au sio mmasai,labda ni kabila jingine kama mngoni au mjita au msukuma hatamwelewa.Kwa hiyo,lugha ya Kiswahili imekuwa ni lugha ya kuwaunganisha watanzania pamoja.Na ndio maana tunasema Tanzania ni nchi ya amani,nchi ya umoja,aah!umoja huu umetokana na jinsi ambavyo watanzania (tume)tunatumia hii lugha ya Kiswahili katika mawasiliano,katika maisha ya kila siku.

English translation:

First of all, I would like to welcome you to Tanzania. Tanzania is in one of the East African countries, and it is a peaceful country. Swahili is our national language and it is the language which unites all Tanzanians. We use Swahili in our everyday communication, in the workplace, at schools, at home and in situations and ceremonies where people gather. We are happy that Tanzania is the land of peace and love, and all Tanzanians have been united by this one language that is Swahili. Tanzania has more than one hundred tribes and from those tribes, we have more than one hundred tribal languages. Even though people have their own tribal languages, we have all been united by Swahili. Here I mean that we have the Maasai tribe, Chagga tribe, Ngoni tribe, Gita tribe, Sukuma tribe and others. Each tribe has its own language. For example, the Maasai tribe has its own language which we call Maasai; the Chagga tribe has Chagga, and the same for the Ngoni and Sukuma tribes. When these people meet, for example, as when a Chagga person meets a Sukuma person, because their languages are different, obviously they will use Swahili to communicate. If a Chagga or Maasai uses his language to talk to a person who is not a Chagga or Maasai, maybe from the Ngoni or Gita or Sukuma tribes, they will not understand each other. So Swahili is the language which unites all people. That is why we say Tanzania is the land of peace and unity, and this unity is the result of sharing the Swahili language in our everyday communications.

About CultureTalk: CultureTalk is produced by the Five College Center for the Study of World Languages and housed on the LangMedia Website. The project provides students of language and culture with samples of people talking about their lives in the languages they use everyday. The participants in CultureTalk interviews and discussions are of many different ages and walks of life. They are free to express themselves as they wish. The ideas and opinions presented here are those of the participants. Inclusion in CultureTalk does not represent endorsement of these ideas or opinions by the Five College Center for the Study of World Languages, Five Colleges, Incorporated, or any of its member institutions: Amherst College, Hampshire College, Mount Holyoke College, Smith College and the University of Massachusetts at Amherst.

© 2003-2008 Five College Center for the Study of World Languages and Five Colleges, Incorporated